East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi Wakimbizi wa Sudan Kusini katika Ushairi wa Kiswahili

*Edward Ekadeli Lokidor*[1*]

[1] Chuo Kikuu Kishirikishi cha Turkana, S. L. P. 69-30500, Lodwar, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: lokidorbalozi@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*23 Februari 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ushairi wa Kiswahili, Ugumu wa Ushairi, Wanafunzi Wakimbizi, Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, Mbinu na Nyenzo za Kufundisha.*

## IKISIRI

Utafiti huu unaeleza changamoto zinazowakumba wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu ulilenga kuchunguza changamoto zinazokumba wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini katika ushairi wa Kiswahili katika shule ya upili. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilielekeza utafiti huu. Utafiti huu ulifanywa katika shule ya upili ya Fanaka (jina la msimbo) katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma, Kaskazini Magharibi mwa Kenya. Data ilikusanywa kupitia mahojiano, uchunzaji na uchanganuzi wa matini. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini wanakabiliwa na changamoto ya ugumu wa kujibu maswali ya ushairi. Changamoto ya ugumu wa ushairi kwa wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini imetokana na mtazamo hasi kuwa ushairi ni mgumu, ukosefu wa miongozo ya ushairi, ukosefu wa vitabu teule vya ushairi, na walimu kutotumia mbinu na nyenzo mwafaka za kufundisha ushairi. Utafiti umetoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha ufundishaji wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Aidha, utafiti huu unatoa mchango kwa ufundishaji na ujifunzaji wa ushairi wa Kiswahili kwa wanafunzi wa kigeni wanaojifunza Kiswahili.

**APA CITATION**

Lokidor, E. E. (2023). Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi Wakimbizi wa Sudan Kusini katika Ushairi wa Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 16-22. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106.

**CHICAGO CITATION**

Lokidor, Edward Ekadeli. 2023. “Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi Wakimbizi wa Sudan Kusini katika Ushairi wa Kiswahili”. *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 16-22. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

**HARVARD CITATION**

Lokidor, E. E. (2023) "Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi Wakimbizi wa Sudan Kusini katika Ushairi wa Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 16-22. doi: 10.37284/jammk.6.1.1106.

**IEEE CITATION**

E. E. Lokidor, "Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi Wakimbizi wa Sudan Kusini katika Ushairi wa Kiswahili", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 16-22, Feb. 2023.

**MLA CITATION**

Lokidor, Edward Ekadeli. "Changamoto Zinazowakabili Wanafunzi Wakimbizi wa Sudan Kusini katika Ushairi wa Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Feb. 2023, pp. 16-22, doi:10.37284/jammk.6.1.1106.

## UTANGULIZI

Ushairi ni utanzu mkongwe sana wa fasihi andishi ya Kiswahili ambao umetumiwa kama jukwaa la kueleza tajiriba ya maisha ya binadamu (Oyinda & Lokidor, 2021; Shitemi, 2010). Vile vile, ushairi umekuwa dafina ya kupitisha maadili kwa jamii pana (Swaleh & Timammy, 2019). Hata hivyo, kuna imani potofu ambayo imesakini miongoni mwa watu kuwa ushairi ni mgumu (Njogu & Chimerah, 2000). Imani hii potofu kuwa ushairi ni mgumu imeenea mno miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Mtazamo huu hasi kuwa ushairi ni mgumu mno umewafanya wanafunzi kuogopa ushairi (Walla, 1988). Isitoshe, kuna baadhi ya walimu wa Kiswahili ambao pia wameishia kutekwa nyara na mtazamo huu hasi kuwa ushairi ni mgumu (Mohamed, 1990).

Ugumu wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya umepelekea tafiti kadhaa kufanywa kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa ushairi. Mwangi (2005) alichunguza misingi ya ugumu wa mashairi katika shule za upili. Utafiti wa Mwangi unawiana na utafiti huu japo mazingira na muktadha zinatofautiana. Kwani utafiti huu ulifanyika katika shule ya upili katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma ambapo Kiswahili ni lugha geni kwa wanafunzi wakimbizi. Nao Iyaya, Kobia na Luganda (2016) walibaini ukosefu wa nyenzo za ufundishaji kama changamoto inayotinga ufundishaji wa ushairi katika shule za upili. Mukoya (2019) alichunguza namna walimu wanavyofundisha kipengele cha mtindo katika ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Mukoya anapendekeza kuwa walimu watumie mbinu zitakazowafanya wanafunzi kupenda somo la ushairi. Ingawa tafiti hizi zimechunguza changamoto za ushairi katika shule za upili, hazijachunguza changamoto zinazokumba wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini katika ushairi.

Utafiti huu ulichunguza changamoto zinazowakumba wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini katika ushairi katika shule za upili za Kakuma nchini Kenya. Utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi kutoka Sudan Kusini wanakabiliwa na changamoto katika ushairi kiasi cha kupata ugumu kujibu maswali ya ushairi katika mtihani. Utafiti umetoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha ufundishaji wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya. Aidha, utafiti huu unatoa mchango kwa ufundishaji na ujifunzaji wa ushairi wa Kiswahili kwa wageni.

## NADHARIA UCHANGANUZI MAKOSA

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Corder (1967). Kulingana na nadharia hii, kuna mambo mengi yanayosababisha makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili (L2) bali na athari ya lugha ya kwanza (L1). Nadharia hii inaweka bayana mikakati inayotumiwa na wanafunzi kujifunza L2. Aidha, nadharia hii inatambua sababu ya makosa wanayofanya wanafunzi wakati wa kujifunza lugha ya pili.

Makosa ya wanafunzi katika kujifunza lugha yanaweza kutumiwa na walimu kukarabati makosa hayo na kuboresha uelewa wa wanafunzi katika L2

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

(Norrish, 1983). Aidha makosa ya wanafunzi katika kujifunza L2 yana manufaa kwa walimu kwani yanaweza kuwasaidia walimu kutathmini ubora au udhaifu wa mbinu na vifaa vya ufundishaji wa L2 darasani (Corder, 1974). Kwa hivyo nadharia hii ilisaidia katika kutathmini mbinu na vifaa ambavyo walimu hutumia katika kufundisha ushairi katika shule za upili katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma.

Mihimili miwili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ndiyo ilitumiwa katika kazi hii. Mosi, wakati mwanafunzi anajifunza lugha huweza kufanya makosa. Kwa mfano katika kujibu maswali ya ushairi huenda mwanafunzi akafanya kosa kwa sababu ya kukosa kuelewa vipengele anuwai vya ushairi au kukosa umilisi katika stadi ya kujibu maswali ya ushairi. Pili, ni jambo la kawaida kwa mwanafunzi kufanya makosa wakati anajifunza L2 na kwa hivyo mwalimu hafai kumwadhibu mwanafunzi au kufanya mwanafunzi kuonekana duni. Hata hivyo mwalimu anafaa kumsaidia mwanafunzi kutambua makosa yake ili kupata kuelewa zaidi.

Nadharia hii ilitumiwa kubaini makosa ambayo wanafunzi hufanya wanapojibu maswali ya ushairi katika karatasi ya pili ya Kiswahili. Kwa wakati uo huo nadharia ilisaidia kubaini mbinu ambazo walimu hutumia katika kufundisha mashairi katika shule za upili.

## METHODOLOJIA

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo uliniwezesha kukusanya data katika mazingira halisi ya shule ya upili katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma, Kaskazini Magharibi mwa Kenya. Aidha, muundo wa kimaelezo ulitumiwa kwa sababu sikuwa na udhibiti juu ya watafitiwa na matukio katika shule ya upili ya wakimbizi katika kambi ya Kakuma, Kaskazini Magharibi mwa Kenya. Data kutoka nyanjani na maktabani zilichanganuliwa na kwa njia ya maelezo.

### Njia za Utafiti

Utafiti huu ulitumia uchunzaji, mahojiano na uchanganuzi wa matini kukusanya data.

#### *Mahojiano*

Mahojiano yaliwalenga wanafunzi wakimbizi 12 kutoka Sudan Kusini wa kidato cha tatu na nne, na walimu 3 wa Kiswahili. Kabla ya kuanza mahojiano niliwaeleza wahusika kuhusu lengo la utafiti na kuomba idhini yao kushiriki kwa kutia sahihi kwenye fomu ya dhamiri.

Niliwahoji wanafunzi wakimbizi 12 kutoka Sudan Kusini na walimu 3 wa Kiswahili katika shule ya upili katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma. Mahojiano yalilenga kuzua majibu kuhusu mbinu na vifaa vya kufundishia mashairi na mielekeo ya wanafunzi kuhusu ushairi wa Kiswahili. Mahojiano haya yalichukua dakika 45 kwa kila mtafitiwa. Mahojiano yalifanywa katika darasa maalumu ambalo halikuwa na kelele. Mahojiano haya yalifanywa mara mbili mwanzoni na mwishoni mwa kipindi cha utafiti nyanjani.

Jukumu langu katika mahojiano lilikuwa kusikiliza kwa wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini na walimu wa Kiswahili wakitoa kauli zao. Hata hivyo kuna wakati ambao nilionyesha hisia labda za kutoamini kauli fulani za watafitiwa. Kupitia mahojiano nilipata data iliyolenga maswali ya utafiti huu.

#### *Uchunzaji*

Uchunzaji ulifanywa katika kidato cha tatu na nne katika vipindi vya Kiswahili kwa muhula mzima. Mwongozo wa uchunzaji ulitumiwa kuelekeza uchunzaji darasani. Lengo la uchunzaji lilikuwa kubaini namna walimu wanafundisha ushairi, nyenzo za kufundishia na ushiriki wa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa mashairi. Nilinakili matukio yaliyojiri darasani katika kitabu changu cha matukio nyanjani.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

***Uchanganuzi wa Matini***

Matini kuhusu tafiti mbalimbali kuhusu mashairi yalichanganuliwa maktabani. Pia, ripoti ya mtihani wa kitaifa wa fasihi (KNEC, 2019) kuhusu sehemu ya ushairi ilichanganuliwa. Vile vile, silabasi ya Kiswahili kwa shule za upili na makala ya wanafunzi. Lengo la kuchanganua matini lilikuwa kubaini namna mashairi yanafundishwa katika shule za upili, mtazamo wa wanafunzi kuhusu ugumu wa ushairi na matatizo yanayowakumba wanafunzi katika kujibu maswali ya ushairi katika mtihani wa kitaifa.

***Watafitiwa***

Watafitiwa wa utafiti huu walikuwa wanafunzi 12 kutoka Sudan Kusini; wavulana 7 na wasichana 5. Walimu walikuwa 3 wa Kiswahili; kiume 2 na wa kike 1. Wanafunzi hawa walikuwa katika kidato cha tatu na kidato cha nne katika shule ya upili ya Fanaka (Jina la msimbo) katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma, kaskazini magharibi mwa Kenya. Walimu wa Kiswahili walioshiriki katika utafiti huu walikuwa Wakenya.

## MATOKEO

Utafiti huu ulilenga kuchunguza changamoto zinazowakumba wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu ulibaini kwamba wanafunzi kutoka Sudan Kusini wana matatizo katika ushairi wa Kiswahili kiasi cha kupata ugumu kujibu maswali ya ushairi. Uchanganuzi wa data ya mahojiano, uchunzaji na uchanganuzi wa matini ya maktabani ulizua maudhui yafuatayo:

### Ushairi ni Mgumu

Uchambuzi wa data ya mahojiano ulidhihirisha kwamba wanafunzi kutoka Sudan Kusini wana mtazamo hasi kwamba ushairi ni mgumu. Baadhi ya kauli zao zinazodhihirisha kuwa wana mtazamo hasi kuwa ushairi ni mgumu kiasi cha kuogopa maswali ya ushairi ni:

| | |
|---|---|
| Mtafitiwa 1: | *Ushairi huwa mgumu sana kwangu. Huwa najaribu kusoma lakini sielewi na nikiuliza wenzangu nao wanasema ni mgumu.* |
| Mtafitiwa 2: | *Maswali ya shairi huwa magumu. Huwa naomba isiwe swali la lazima katika mtihani maana najua nitapata alama kidogo.* |
| Mtafitiwa 3: | *Mashairi huwa magumu sana kuelewa. Mimi huwa sifanyi swali la ushairi maana najua nitapata 'zero' (sufuri).* |
| Mtafitiwa 4: | *Hata kwa 'group discussion' (makundi ya majadiliano). Ni ngumu sana si rahisi upate wanafunzi wakijadili maswali ya mashairi.* |

Kauli hizi zinaonyesha namna mtazamo hasi unawafanya wanafunzi kuogopa maswali ya ushairi na hata kukosa kujadili maswali ya ushairi katika makundi yao. Data hii ya mahojiano na data kutoka uchunzaji darasani ilionyesha kwamba wanafunzi hawasomi ushairi mara nyingi na wanaogopa kujibu maswali ya ushairi darasani kwani wanaona maswali ya ushairi kuwa magumu. Mtazamo hasi kuwa ushairi ni mgumu unadhibitishwa na ripoti ya KNEC ( k.h.j) inaonyesha kwamba wanafunzi wengi hukwepa swali la ushairi katika mtihani na iwapo swali la lazima ni ushairi katika fasihi, wanafunzi hawa huishia kupata alama za chini mno katika mtihani wa fasihi. Hata hivyo mtazamo kuwa ushairi ni mgumu unaweza kubadilishwa na walimu kwa kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zitakazowafanya wanafunzi kuwa na mitazamo changa katika ushairi (Odaga, 1985).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

### Ukosefu wa Miongozo Bora ya Uchambuzi wa Ushairi

Utafiti huu ulibaini kwamba kuna vitabu vichache mno vinavyochambua vipengele anuwai vya ushairi kwa mapana na marefu. Mtafiti mmoja alitoa kauli hii:

> *" Kwa maktaba hakuna vitabu vya ushairi ambavyo vinaweza kutusaidia kuelewa ushairi vizuri. Unajua tukijua ushairi vizuri tutaweza kujibu maswali vizuri na kupata alama bora katika ushairi"*

Aidha ilibainika wazi kwamba kuna baadhi ya miongozo ya ushairi haijatazama masuala ya kimsingi ya uchambuzi wa ushairi kama vile aina ya mashairi, bahari, istilahi za ushairi, namna ya kujibu maswali ya ushairi na mifano ya maswali ya ushairi. Kama alivyosema mtafitiwa mmoja:

> *"Miongozo ya mashairi ambayo nimeona haielezi vizuri namna ya kujibu maswali ya ushairi. Isitoshe, ina maneno magumu ambayo yanachanganya."*

Kauli ya mtafitiwa huyu inaoungwa mkono na ripoti ya KNEC kwamba miongozo mingi ya ushairi inaeleza vipengele vya uchambuzi wa ushairi kwa misamiati tofauti tofauti hivyo basi kuwachanganya wanafunzi. Hii ina maana kwamba wanafunzi wanashindwa kubaini istilahi ipi ndio sahihi.

### Ukosefu wa Vitabu Teule vya Ushairi

Uchambuzi wa data za mahojiano ulionyesha kwamba hamna vitabu teule vya ushairi vilivyoidhinishwa kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa KCSE. Watafitiwa walitoa kauli hizi:

| | |
|---|---|
| Mtafitiwa wa 1: | *Unajua hakuna vitabu teule vya mashairi viliyopendekezwa kutahiniwa katika mtihani wa fasihi.* |
| Mtafitiwa wa 2: | *Hakuna 'set book' (vitabu teule) vya mashairi ambavyo wanafunzi wanaweza kusoma na kujitayarisha ipasavyo kwa mtihani wa KCSE.* |
| Mtafitiwa wa 3: | *Kama kungekuwa na kitabu teule cha ushairi ambacho wanafunzi watafanya kwa mtihani, ingekuwa rahisi kwetu kuwatayarisha. Lakini vitabu teule kwa sasa ni vya riwaya, tamthilia na hadithi fupi tu.* |

Hali hii ni tofauti na tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi ambazo vitabu fulani huteuliwa na taasisi ya kukuza mitalaa nchini (KICD), ili wanafunzi wafunzwe na kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa KCSE. Kwa hivyo, wanafunzi hawana diwani ya ushairi iliyoteuliwa ili wasome na kuchambua kwa mapana na marefu. Sababu hii huwafanya wanafunzi kukosa uelewa katika ushairi. Hata hivyo walimu wanafaa kuwa wabunifu na kutumia mashairi yaliyomo kwenye vitabu vya lugha, riwaya au kwenye hadithi fupi. Wanaweza kutumia utanzu wa tamthilia kufunza ushairi (Mukoya, 2019).

### Uteuzi Mbaya wa Mbinu na Nyenzo za Ufundishaji Ushairi

Data ya uchunzaji darasani ilidhihirisha kwamba kuna matatizo ya uteuzi nyenzo mwafaka za kufundishia ushairi. Vile vile, kuna baadhi ya walimu wa Kiswahili hawafunzi ushairi japo katika maandalizi yao ya somo hutaja kwamba wamefundisha. Hii imepelekea wanafunzi kutofahamu istilahi mahususi za ushairi kama vile arudhi, vina, mishororo, vipande, mizani, uhuru wa mshairi, muundo wa shairi na matumizi ya lugha katika ushairi. Matokeo haya yanaunga mkono matokeo ya utafiti wa Iyaya, Kobia na Luganda (2016) waliobaini kwamba walimu katika shule za upili hawatumii nyenzo katika kufundisha ushairi na vipengele vya ushairi vinavyowatatiza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

wanafunzi ni misamiati migumu, mbinu za lugha na lugha ya nathari.

Pia utafiti huu ulibaini kwamba walimu katika kambi ya wakimbizi hawatumii mifano ya mashairi katika ufundishaji wa ushairi. Data ya mahojiano ilidhibitisha kwamba wanafunzi hawapewi mazoezi ya kujibu maswali ya ushairi katika vipindi vya Kiswahili darasani. Kwa mfano watafitiwa walitoa madai yafuatayo:

| | |
|---|---|
| Mtafitiwa 1: | *Si rahisi tupewe zoezi la mashairi darasani au kama kazi ya ziada ya kufanya nyumbani.* |
| Mtafitiwa 2: | *Walimu wangekuwa wanakuja na mifano kadhaa ya mashairi darasani tunaweza kuelewa ushairi.* |

Hii ina maana kwamba wanafunzi wanakosa uelewa wa namna ya kujibu maswali ya ushairi kwani hawapewi maswali ya ushairi. Wanafunzi wataweza kurekebisha makosa yao iwapo watapewa mazoezi ya ushairi ili kupima udhaifu wa wanafunzi katika ushairi. Baada ya kubaini udhaifu wa wanafunzi katika ushairi, walimu wataweza kuwaelekeza wanafunzi jinsi ya kujibu maswali ya ushairi ipasavyo. Kwa njia hiyo wanafunzi wataweza kuelewa ushairi vizuri na kufanya vyema katika mtihani wa kitaifa. Hali inaweza kubadilishwa kwa walimu kuteua nyenzo mwafaka za ufundishaji na ujifunzaji katika kipindi cha somo la ushairi (Ayot, 1986). Kwa namna hiyo wataweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa ushairi vizuri.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulichunguza changamoto zinazowakumba wanafunzi wakimbizi kutoka Sudan Kusini katika ushairi wa Kiswahili katika shule ya upili katika kambi ya wakimbizi ya Kakuma. Utafiti huu ulibaini kwamba wanafunzi kutoka Sudan Kusini wanakabiliwa na changamoto ya ugumu wa kujibu maswali ya ushairi. Ugumu huu umetokana na mtazamo hasi kuwa ushairi ni mgumu, ukosefu wa miongozo ya ushairi, ukosefu wa vitabu teule za ushairi na walimu kufanya uteuzi mbaya wa mbinu na nyenzo za ufundishaji.

Kwa kurejelea nadharia ya uchanganuzi wa makosa walimu wanafaa kuwapa wanafunzi maswali mara kwa mara ili kubaini makosa ya wanafunzi. Baada ya kubaini makosa wanayofanya wanafunzi katika ushairi, walimu wataweza kuwasaidia wanafunzi kujua namna ya kujibu maswali ya ushairi vyema. Pia kupitia kutambua makosa ya wanafunzi katika kujibu maswali, walimu wataweza kuteua na kutumia mbinu na nyenzo mwafaka za kufundisha ushairi. Kwa mfano, kutumia mbinu mwelekeo mseto wa ufundishaji katika ufundishaji wa Kiswahili ambapo mwalimu anaweza kufundisha ushairi katika somo la lugha kama vile ufahamu ambao ni ushairi (KIE, 2006). Kwa njia hiyo wanafunzi wataweza kuwa na mtazamo changa katika ushairi. Hii ina maana kwamba walimu wa fasihi wanafaa kuandaa vipindi vya ushairi mara kwa mara na kutumia vifaa bora vya kufundisha ushairi ili wanafunzi waelewe ushairi vizuri.

## MAREJELEO


Ayot, H.O (1986). Instructional Materials for Educational Communication and Technology. First Edition. Kenyatta University, Kenya.

Corder, S. P. (1967). The Significance of Learners' Errors. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, 5, 161-170.

Corder, S.P. (1974). Error Analysis, In Allen, J.L.P. and Corder, S.P. (1974). Techniques in Applied Linguistics. Oxford: Oxford University Press

Iyaya , R., Kobia, J., & Luganda, M. (2016). Uchanganuzi wa Mambo Yanayoathiri Ufundishaji wa Ushairi Katika Shule za Upili Nchini Kenya, *Mara Research Journal of Kiswahili 1(1)*, 18-36.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1106

Mohamed, S. A. ( 1990). Mfumo wa 8:4:4 Mbinu na Mazoezi ya Ushairi. Nairobi. Evans Brothers (Kenya) Ltd.

Mukoya, H. (2019). *Ufundishaji wa Ushairi kwa Kutumia Tamthilia Katika Shule Za Upili Kenya: Uchunguzi Kifani kaunti ndogo ya Teso Kaskazini*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kibabi (haijachapishwa)

Mwangi, J. (2005). *Ufundishaji na Ujifunzaji wa Ushairi katika Shule za Upili*.Tasnifu ya uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K., & Chimerah, R. (2000) Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Norrish, J. (1983). Language learners and their Errors. London: Macmillan Press.

Odaga, A. (1985). *Literature for children and Young People in Nairobi.* Nairobi University Press.

Oyinda, P., & Lokidor, E. (2021) *Mwongozo wa Ushairi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Dilev Publication Limited.

KNEC (2019). *Ripoti ya utahini ya Karatasi ya 3, Fasihi* .

Shitemi, N. (2010). *Ushairi wa Kiswahili; kabla ya karne ya ishirini*. Eldoret :Moi University Press.

Swaleh, A., & Timammy, R. (2019). Literature as medium for Moral Instruction: A Swahili/Islamic Analysis of Ahmad Nassir's Utenzi wa Mtu ni Utu. Moi University Press.

Taasisi ya Elimu ya Kenya (2006). *Kiswahili sekondari: Mwongozo wa Mwalimu*. Nairobi: K.I.E

Walla, W. (1988). *Malenga wa Ziwa Kuu, Maswali na Istilahi za Kifasihi*, Nairobi: East African Education Publishers.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.